**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI

## MUHTASARI WA KIKAO CHA DHARURA CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MANISPAA TAREHE 01/12/2021

**MAHUDHURIO**

| | |
|---|---|
| Ndg. Frednand S. Fillimbi | Mwenyekiti |
| Ndg. Rehema C. Kawina | Katibu |
| Ndg. Richard Mtauka | Mjumbe |
| Ndg Kajanja CL | Mjumbe |
| Eng. Wilfred Shimba | Mjumbe |
| Ndg. Beatrice | Mwanasheria |

**WAALIKWA**
Hakuna

**WASIOHUDHURIA KWA TAARIFA**

| | |
|---|---|
| DR. Sebastian N. Siwale | Mjumbe |

**SEKRITALIET**

**Ndg. Moses C.Zahuye**

**Ndg. Tegemeo Bidya**

**AGENDA ZA KIKAO:**

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitsha Agenda
3. Kupitisha matumizi ya Force Account katika Utekelezaji wa miradi ya Uvico
4. Kufunga kikao

**MUHT NA.01/01/12/2021. KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha mwenyekiti ili afungue kikao. Kikao kilifunguliwa mnamo saa 10:30 jion . Mwenyekiti alianza kwa kuwakaribisha wajumbe wote na kuwaomba waanze kujadili agenda zilizopo mezani. \

**MUHT NA.02/01/12/2021. KUTHIBITISHA AGENDA**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti na ndipo mwenyekiti alipo wahoji wajumbe kama wanazipokea na kama wapo tayali kujadili ajenda zilizopo mezani ndipo wajumbe wote kwa pamoja walikubali kuwa agenda zilizoletwa mezani zijadiliwe

**MUHT NA.03/01/12/2021 MAOMBI YA KIBARI CHA KUTUMIA FORCE ACCOUNT**

**Wajumbe walipata nafasi ya kusomewa sababu za msingi zinazopelekea Taasisi kuamua kutumizi ya njia ya force Acount katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo uwasilishaji huo ulifanywa na katibu wa bodi na sababu hizo ni**

**(a) pale kazi za ujenzi zinapokuwa zimesambaa na zipo maeneo ya mbali na hivyo kusababisha ugumu kumpata mkandarasi atakayeweza kuzifanya kwa gharama halisi kulingana na kazi husika (Mfano, ujenzi au ukarabati wa miundombinu ya choo, darasa, bweni n.k katika maeneo mbalimbali yasiyofikika kirahisi ndani ya Halmashauri moja ambapo ujenzi au ukarabati huo unatakiwa utekelezwe kwa wakati mmoja);**

**(b) pale kazi ya ujenzi au ukarabati inatakiwa kuendelea kufanyika pasipo kuathiri shughuli katika taasisi husika (Mfano, kuendelea na ujenzi au ukarabati wa miundombinu ya shule au chuo wakati shughuli za masomo zikiendelea);**

**(c) pale ambapo athari zisizoepukika zinazoweza kuingilia kazi zitasababishwa zaidi na taasisi husika kuliko Mkandarasi wa nje ya Taasisi (Mfano, ujenzi au ukarabati unaendelea wakati shughuli za taasisi nazo zinaendelea, hivyo muingiliano huu unaweza kuvumilika zaidi na taasisi yenyewe kuliko mkandarasi);**

**(d)pale ambapo kuna dharura zinazohitaji kuchukuliwa hatua ya haraka (Mfano, kuezuka kwa paa la maabara ya kompyuta katika chuo au shule;**

**(e) pale Taasisi inapokuwa na wataalamu wa ujenzi wenye sifa ya kujenga au kukarabati na kusimamia; na**

**(f) pale shughuli ya ujenzi inapokuwa ni sehemu ya kazi za kila siku za**

**FAIDA ZA KUTUMIA FORCE ACCOUNT**

**(a) kupunguza gharama za ujenzi na ukarabati pamoja na kufanya utekelezaji wa mradi kukamilika kwa wakati;**

**(b) kutokuathiri utendaji wa kila siku wa taasisi wakati ujenzi ukiendelea;**

**(c) kukabiliana na dharura zinazohitaji kuchukuliwa hatua za haraka;**

**(d) kutumia wataalam na vifaa vya taasisi ili kupunguza gharama za ujenzi; na**

**(e) kuiwezesha taasisi husika kufanya kazi ya ujenzi na ukarabati kwenye taasisi yake pale ambapo ujenzi ni shughuli za kila siku katika taasisi hiyo**

**Baada ya maelekezo hayo wajumbe kwa pamoja walilidhia matumizi ya force Account kwenye utekelezaji wa miradi hiyo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa alubaini na nane ( 48) yenye jumla ya Tsh 960,000,000/=**

**MUHT NA.04/01/12/2021. KUFUNGA KIKAO**

**Kikao kilifungwa mnamo saa 17:45 kabla ya hapo Mwenyekiti aliikumbusha Sekritariet kuleta taarifa ya mgahawa wa Manispaa kwenye kikao cha Finance lakini pia aliomba ufafanuzi kutoka kwa mtunza hazina wa manispaa juu ya malipo ya posho ya vikao vya bodi ambapo kaimu mweka hazina aliwaahidi wajumbe kulifanyia kazi.**

**IMETHIBITISHWA NA**

................................ ................................

MWENYEKITI KATIBU

TAREHE 01/12/2021